**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 22 - 10 - 2021 KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI**

**WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1 NJAU JOSEPH | - AFISA KILIMO | -M/KITI |
| 2 TEMBA A P | -AFISA MANUNUZI | -KATIBU |
| 3 MR MKANA M MKANA | -AFISA MAZINGIRA | -MJUMBE |
| 4 Bi ROSEMERY MSASI | -AFISA ELIMU | -MJUMBE |
| 5 ENG BRIGHTON KISHEO | -MHANDISI WA MJI | -MJUMBE |

**WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

1 DR TULITWENI MWINUKA -MGANGA MKUU WA MJI

**WAALIKWA**

1. MANSUETHA MBENA -MWANASHERIA WA MJI

Agenda:

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasri wa tarehe 11/10/2021
4. Kupitia na kuidhinisha punguzo la gharama Manunuzi ya kawaida idara tofauti yaliyofanyika kwenye Mfumo wa TANePS.
5. Kupitia na kuidhinisha Manunuzi ya kawaida idara tofauti yaliyofanyika kwenye Mfumo wa TANePS.
6. Kupitia na kuidhinisha taarifa ya tathmini zabuni ya uwekwzaji kitovu cha mji mita za mraba 2860
7. Maombi ya kupitisha matumizi ya fedha za ujenzi wa madarasa na hospitali ya wilaya kwa kutumia njia ya force accounts
8. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
9. Kufunga kikao.

**Agenda Na 01/ BZ 07 / 2021**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 5 30 Asubuhi.

**Agenda Na 02/ BZ 07/ 2021 KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zote wajumbe wa Bodi zilithibitishwa kuwa Agenda sahihi

**Agenda Na 03/ BZ 07 / 2021 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASRI WA TAREHE 11/10/2021**

Wajumbe walipitia na kufanya masahihisho yafuatayo, mwalikwa wa kikao Afisa TEHAMA Amina Hoza ajumuishwe kwenye majina ya waalikwa

**AGENDA NA: 04/ BZ. 07 / 2021; KUPITIA NA KUIDHINISHA PUNGUZO LA GHARAMA MANUNUZI YA KAWAIDA IDARA TOFAUTI YALIYOFANYIKA KWENYE MFUMO WA TANEPS.**

**UNUNUZI WA CHAKULA IDARA YA AFYA**

Katibu aliwasilisha kuwa mzabuni M/S AKO GROUP CO. LTD alitwa kwa ajili ya majadiliano na amekubali kupunguza bei ya chakula na kuwa shilingi 8000/= kwa chakula na shilingi 3500/= kwa chai. Baada ya kupitia wajumbe wa bodi walidhia mabadiliko hayo na kufanya jumla ya chakula kuwa shilingi 1,840,000/= badala ya 2,171,200/=

**UNUNUZI WA CHAKULA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII**

Katibu aliwasilisha kuwa mzabuni M/ M/S CHRIJO FOOD PRODUCTION alitwa kwa ajili ya majadiliano na amekubali kupunguza bei ya chakula na kuwa shilingi 8000/= kwa chakula na shilingi 3000 kwa chai. Baada ya kupitia wajumbe wa bodi walidhia mabadiliko hayo na kufanya jumla ya chakula kuwa shilingi 960,000/= badala ya 1,200,000/=

**AGENDA NA: 05/ BZ. 07 / 2021; KUPITIA NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA KAWAIDA IDARA TOFAUTI YALIYOFANYIKA KWENYE MFUMO WA TANEPS.**

**UNUNUZI WA SHAJALA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII**

M/S SALIS COMPANY LIMITED aliomba kwa 2,00,700/=
M/S CARE QUALITY GENERAL SUPPLIES aliomba kwa 2,580,660/=
M/S FIREBRAND TECHNOLOGY aliomba kwa 2,292,150/=
M/S KIBARA GENERAL SUPPLIES aliomba kwa 2,398,000/=

Bodi ya zabuni imempitisha M/S SALIS COMPANY LIMITED aliyeomba kwa Tsh. 2,00,700/= kupewa kazi hiyo kwa kuwa amekidhi vigezo

**UNUNUZI WA DESKTOP COMPUTER IDARA YA AFYA**

M/S LUNA GENERAL SUPPLIES aliomba kwa 2,100,000/=
M/S GHP COMPANY LIMITED aliomba kwa 2,830,584/=
M/S FIREWORKS SOLUTION aliomba kwa 2,112,200/=
M/S KIBARA GENERAL SUPPLIES aliomba kwa 2,230,000/=
M/S SIM ELECTROCOM TANZANIA LIMITED aliomba kwa 1,841,744/=

Bodi ya zabuni imempitisha M/S SIM ELECTROCOM TANZANIA LIMITED aliyeomba kwa Tsh. 1,841,744/= kupewa kazi hiyo kwa kuwa amekidhi vigezo

**AGENDA NA. 04 BZ 07 2021: KUPITIA NA KUIDHINISHA PUNGUZO LA GHARAMA MANUNUZI YA KAWAIDA IDARA TOFAUTI YALIYOFANYIKA KWENYE MFUMO WA TANEPS.**

**UNUNUZI WA CHAKULA IDARA YA AFYA**

Katibu aliwasilisha kuwa mzabuni M/S AKO GROUP CO LTD alitwa kwa ajili ya majadiliano na amekubali kupunguza bei ya chakula na kuwa shilingi 8000/= kwa chakula na shilingi 1500/= kwa chai. Baada ya kupitia wajumbe wa bodi waliidhia mabadiliko hayo na kufanya jumla ya chakula kuwa shilingi 1,840,000/= badala ya 2,111,200/=

**UNUNUZI WA CHAKULA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII**

Katibu aliwasilisha kuwa mzabuni M/ M/S CHRISTFOOD PRODUCTION alitwa kwa ajili ya majadiliano na amekubali kupunguza bei ya chakula na kuwa shilingi 8000/= kwa chakula na shilingi 1000 kwa chai. Baada ya kupitia wajumbe wa bodi waliidhia mabadiliko hayo na kufanya jumla ya chakula kuwa shilingi 960,000/= badala ya 1,200,000/=

**AGENDA NA. 05 BZ 07 2021. KUPITIA NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA KAWAIDA IDARA TOFAUTI YALIYOFANYIKA KWENYE MFUMO WA TANEPS.**

**UNUNUZI WA SHAJALA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII**

M/S SALIX COMPANY LIMITED aliomba kwa 2,00,700/=
M/S CARE QUALITY GENERAL SUPPLIES aliomba kwa 2,580,000/=
M/S FIREBRAND TECHNOLOGY aliomba kwa 2,292,150/=
M/S KIBARA GENERAL SUPPLIES aliomba kwa 2,308,000/=

Bodi ya zabuni imempitisha M/S SALIX COMPANY LIMITED aliyeomba kwa Tsh 2,00,700/= kupewa kazi hiyo kwa kuwa amekidhi vigezo

**UNUNUZI WA DESKTOP COMPUTER IDARA YA AFYA**

M/S LUNA GENERAL SUPPLIES aliomba kwa 2,100,000/=
M/S GHP COMPANY LIMITED aliomba kwa 2,830,584/=
M/S FIRE WORKS SOLUTION aliomba kwa 2,113,200/=
M/S KIBAJRA GENERAL SUPPLIES aliomba kwa 2,210,000/=
M/S SIM ELECTROCOM TANZANIA LIMITED aliomba kwa 1,841,744/=

Bodi ya zabuni imempitisha M/S SIM ELECTROCOM TANZANIA LIMITED aliyeomba kwa Tsh. 1,841,744/= kupewa kazi hiyo kwa kuwa amekidhi vigezo.

**AGENDA NA: 06/ BZ. 07 / 2021: KUPITIA NA KUIDHINISHA TAARIFA YA TATHMINI ZABUNI YA UWEKEZAJI KITOVU CHA MJI SM MITA ZA MRABA**

Katibu aliwasilsha kama ifuatavyo;

## UTANGULIZI

Kitengo cha Ugavi kilipokea Dokezo kutoka kwa Mkurugenzi fikiwa na maombi ya kumtafuta mwekezaji kwa ajili ya uendelezaji wa eneo la wazi katika eneo la kitovu cha Mji.

Halmashauri ya Mji iliweza kutoa tangazo la kazi hiyo tarehe 30.08.2021 na ufunguzi huo ulifanyika tarehe 14.09.2021

Zabuni hiyo iliombwa na mwekezaji mmoja tu ambae ni

1. Shilla Jonathan Nkurlu ambae alieleza kuwa atakuwa anawasilisha Tsh- 1,276,000 kwa mwezi

Kamati ya tathmini iliundwa na Mkurugenzi kwa kuhusisha wataalamu wafuatao:-

1. Filemon J.Siriwa-Mhasibu - Mwenyekiti
2. Issa A Issa TARURA Kibaha Mji-Mhandisi-Katibu
3. Adolph L.Msangi-MjumbE-Afisa Biashara-Mjumbe

- **UCHAMBUZI WA KINA**

Kamati ya tathmini ilieleza kuwa uchambuzi wa kina ***detailed evaluation*** ulizingatia tangazo la zabuni,kwamba waombaji wa zabuni walitakiwa kuambatisha taarifa kulingana na masharti ya waombaji

- **MAPENDEKEZO YA KAMATI YA TATHMINI**

Kamati ya tathmini ilimpendekeza Mwekezaji Shilla Jonathan Nkurlu kupewa kazi hiyo ya uwekezaji wa muda eneo la wazi kwa gharama ya Tsh 460,424,050 na malipo ya Kiasi cha Tsh 1,276,000 kwa mwezi

Vile vile kamati iliweza kushauri kuitwa kwa Mwekezaji huyo aliyependekeza kupewa kazi hiyo kufanya nae majadiliano ya kuhusu ujenzi wa vibanda alivyoambatisha katika mchoro wake ambapo kutokana na mchoro huo unaonesha kuwa amekusudia kuweka uwekezaji wa ujenzi wa vibanda /Frems ambavyo vina gharama ya Tsh 460,424,050 ambapo kwa mujibu wa uwekezaji wa eneo hilo palitakiwa kuwe na eneo kwa ajili ya nyama choma na vinywaji pamoja na eneo la michezo kwa watoto

Pia kamati ya tathmini inashauri muda wa uwekezaji katika eneo hilo uendane na gharama ya uwekezaji wa eneo hilo kwa kuzingatia mita za mraba zitakazopangishwa katika eneo hilo

Pia suala la muda pia lifanyiwe majadiliano

**MAONI YA KITENGO CHA MANUNUZI**

Kitengo cha manunuzi kiliweza kuridhia mapendekezo ya Kamati ya tathmini.

**MAONI YA BODI YA ZABUNI**

Bodi ya zabuni baada ya kupitia taarifa ya kitengo cha manunuzi na taarifa ya tathmini iliamua kuwa Mzabuni husika aitwe kwa ajili ya majadiliano ili aendane na masharti ya tangazo kuwa eneo husika ni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuuzia vinywaji vikali na laini, nyama choma, chakula, michezo ya watoto na sehemu za kupumzika.

**AGENDA NA: 01/BZ 07/2021; MAOMBI YA KUPITISHA MATUMIZI YA FEDHA ZA UJENZI WA MADARASA NA HOSPITALI YA WILAYA KWA KUTUMIA NJIA YA FORCE ACCOUNTS.**

Katibu aliwasilisha kuwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha imepokea Fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya Ujenzi wa Madarasa 47 ya shule za Msingi na inatarajiwa kupokea Fedha za Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya awamu ya III.

Katibu alieleza kuwa Fedha za Ujenzi wa Madarasa 47 ni shilingi 940,000,000/= ni fedha za maendeleo ya Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya Uviko na fedha za Ujenzi wa Hospitali ni fedha za ruzuku shilingi 800,000,000/= Baada ya maelezo hayo Katibu alieleza kuwa fedha hizo zinatakiwa kutumiwa kwa njia ya Manunuzi ya Force Accounts. Hii ni kwa mujibu wa waraka kutoka Katibu Mkuu TAMISEMI na Semina elekezi ya tarahe 18/01/2021 iliyofanyika kwa Katibu Tawala Mkoa wa Pwani na pia fedha hizo zitatumwa moja kwa moja mashuleni ili wananchi washirikishwe.

Wajumbe kwa pamoja baada ya kupata taarifa hiyo walikubaliana na mapendekezo hayo kuwa njia ya Manunuzi itumike Force Account kama ilivyoagizwa katika muongozo.

**AGENDA NA. 08/CZ 07/2021; MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Hakukuwa na mengineyo.

**AGENDA NA.; 08/BZ 07/2021; KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 6:30 Asubuhi.

| | |
|---|---|
| ............................ | ............................ |
| MWENYEKITI | KATIBU |